

# MTIHANI WA DARASA LA SITA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA 2019

## KISWAHILI

**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

**1. Hakikisha umeandika**

(i) Jina la

(ii) Jina la shule yako

Muda: Saa 1 Dak. 40

**Soma vifungu vifuatavyo, vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne.**

**Chagua jawabu lifaalo zaidi.**

Mzee Mashaka hakuzaliwa 1 kamwe. Alizaliwa 2 na macho kamili. Tena 3 kama binadamu yeyote wa kawaida. Lakini 4 kupita siku kadhaa, 5 ikawa tofauti. Inasemekana mzee Mashaka alihusika katika 6 barabarani. Daladala alimosafiria iligongana 7 na trela la kubeba 8. 9 wengi walipoteza maisha yao papo kwa hapo. Walioaga dunia walipelekwa katika 10 ya kaunti ya Peponi na kuhifadhiwa huko. 11 nao walilazwa katika hospitali ya rufaa jijini Peponi. 12 umeiandama familia ya mzee Mashaka, wameshindwa kabisa kulipa 13 ya hospitali. Ni kweli kwamba 14 la mnyonge haliendi joshi, msaada wa dharura unahitajika kuisaidia 15 hili isiyu na mbele wala nyuma.

- |                       |                |                     |                    |
|-----------------------|----------------|---------------------|--------------------|
| 1. A. kiziwi          | B. kipofu      | C. kilema           | D. kibyongo        |
| 2. A. mwenye          | B. alikuwa     | C. akiwa            | D. alipokuwa       |
| 3. A. mbili           | B. moja        | C. mawili           | D. bili            |
| 4. A. badala ya       | B. baada ya    | C. juu ya           | D. licha ya        |
| 5. A. hali            | B. janga       | C. maisha           | D. mambo           |
| 6. A. anasa           | B. jinamizi    | C. uovu             | D. ajali           |
| 7. A. macho kwa macho | B. ana kwa ana | C. upande na upande | D. nyumba na mbele |
| 8. A. viombo          | B. abiria      | C. mizigo           | D. watu            |
| 9. A. mifugo          | B. abiria      | C. maskani          | D. maabiria        |
| 10. A. zahanati       | B. makavazi    | C. mochari          | D. gereza          |
| 11. A. majeruhi       | B. mahafali    | C. mazingaombwe     | D. mahasidi        |
| 12. A. ukwasi         | B. utajiri     | C. ukata            | D. usalama         |
| 13. A. pango          | B. fola        | C. koto             | D. ankara          |
| 14. A. dua            | B. dia         | C. dau              | D. doa             |
| 15. A. jimbo          | B. aila        | C. himaya           | D. gatuzi          |

**Kuanzia swali la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo.**

- |  |                                   |
|--|-----------------------------------|
| 16. Masalheri ni salamu za wakati gani<br>A. jioni<br>C. alasiri   | B. asubuhi<br>D. adhuhuri         |
| 17. Tambua nomino katika ngeli ya U-ZI<br>A. ukuta, ua<br>C. waya, wino  | B. uta, urembo<br>D. upinde, uovu |
| 18. Ni sentensi gani imetumia kivumishi kionyeshi sahihi<br>A. Chupa hiki kimevunjika.<br>B. Kipepeo jkile kimeruka.<br>C. Maziwa hii imemwagika.<br>D. Mkunga huyu ni hodari. |                                   |

19. Tumia -enye kwa usahihi  
 A. Mama mwenye amejifungua anafurahi.  
 B. Maskini mwenye kibanda anasononeka  
 C. Darasa yenye chati huvutia  
 D. Shule yenye anasomea ni kubwa sana.
20. Kitenzi kata katika kauli ya kufanyika itakuwa  
 A. katia B. katakata  
 C. katiwa D. katika
21. Tumia kiulizi sahihi  
 A. Kucheza kugani kunakopendeza?  
 B. Vinyonga vingapi waliokamatwa?  
 C. Chupa ipi kilichojazwa maziwa  
 D. Nzi yupi anayetatiza?
22. Sentensi hii imetumia matumizi ya "ki" vipi  
 Ukifika stanini nipigie simu nije kukusaidia  
 A. ukubwa B. masharti  
 C. kiambishingeli D. udogo
23. Mwalimu Pendo ataenda ng'ambo mwakani  
 Alama ya kuakifisha (') iliyotumika kwenye neno  
 ng'ambo huitwa  
 A. ritifaa B. paradesi  
 C. hisi D. kinukuu
24. Msumeno **huu huu** ndio uliotumiwa kukereza  
 mbao, maneno yaliyopigiwa kijistari ni  
 A. kiashiria kisisitizi B. kiashiria radidi  
 C. kiashiria kioyeshi D. kiashiria halisi
25. Tumia -ingine kujazia pengo  
 Mpunga \_\_\_\_\_ umepandwa wa kwanza  
 umevunwa.  
 A. ingine B. mwengine  
 C. mwingine D. mingine
26. Tumia kihusishi kifaacho  
 Maziwa yamehifadhiwa \_\_\_\_\_ jokofu  
 A. chini ya B. juu ya  
 C. kando ya D. ndani ya
27. Tumia kivumishi sahihi kujazia pengo.  
 Barabara hii \_\_\_\_\_ haikusafikiwa kama  
 ilivyotakiwa.  
 A. bovu B. zuri  
 C. mbāya D. baya
28. Unda maneno kutokana na kitenzi cheza.  
 A. chezea B. mchezo  
 C. mchezaye D. chezewa
29. Tumia kiunganishi bora zaidi  
 Kila abiria amelipa nauli \_\_\_\_\_ mzee Mapunda.  
 A. ingawa B. wala  
 C. bila D. isipokuwa
30. Neno gani kati ya haya iliyotumia irabu tatu  
 A. Gari B. ukurasa  
 C. Mayai D. Kimya

**Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali 31 – 40.**

Bakari Ali Salim,  
 Shule ya msingi hekima  
 S.L.P 20173,  
 Borauhai.  
 12/05/2017.

Kwa Sahibu yangu Mpoto,

Pokea salamu zangu kochokocho nikiwa mwingi wa matumaini kuwa u mzima kama chuma cha pua. Huko shuleni waendelea vipi? Ni matumini yangu unazidi kuuma uzi masomoni bila wahaka wowote. Hata miri huku najikaza kwenye shughuli zangu za masomo kila uchao kwani achanikaye kwenye mpini....

Rafiki yangu Mpoto, nilifurahi sana likizo iliyopita ya Aprili jinsi tulivyoshikiriana kama kinu na mchi tukazifanya kazi zetu za ziada kwa urahisi. Nilifurahia mandhari ya huko kwenu hasa milima ya Mizeituni. Nikafurahia upepo mwanana hasa nyakati za Magharibi. Zipokee shukrani za dhati kwa kuwa wewe, ndugu zako na wazazi wako mlinipa makaribisho na mapokezi shwari nikajihisi kuwa nyumbani wakati huo wote niliokuwa huko.

Madhumuni na azma ya kukuandikia waraka huu ni kukuelezea kuwa ningependa tuendelee na moyo huo huo wa ushirikiano kwa kuwa mkataa wengi ni mchawi. Hii ndiyo sababu ninachukua fursa hii kukualika kwetu wakati wa likizo ijayo ya wezi wa Agosti, ili tufunzane mengi. Huku tu karibu kuanza mitihani yetu ya mwisho wa muhula na hatimaye Mola akiridhia tutafunga skuli kwa takribani majuam mawili. Hivyo basi ikiwezekana unitumie waraka ukinijuza endapo utaweza kuja.

Nafika hapo kwa sasa, asante kwa muda mzuri ulionipa, Nakuombea dua za Jalali jalia zikuandame katika shughuli zote. Tuonane Agosti majaliwa.

Wako wa ulimi na mate,  
Bakari Ali Salim.

- |  |  |
|--|--|
| <p>31. Mwandikiwa barua hii anaitwaje?<br/>A. Bakari Ali Salim    B. Mpoto<br/>C. Borauhai            D. Jalali</p> <p>32. Kwa mujibu wa barua hii unadhani barua hii iliandikwa katika muhula upi<br/>A. wa mwisho            B. wa tatu<br/>C. wa pili                D. wa kwanza</p> <p>33. Barua rasmi huwa na anwani<br/>A. moja                  B. mbili<br/>C. haijulikani          D. haina anwani</p> <p>34. Mwandishi anasisitiza dhana gani katika barua hii<br/>A. uhasama              B. ukatili<br/>C. uzalendo              D. ushirikiano</p> <p>35. Tulivyoshirikiana kama kinu na mchi hii ni fani gani ya lugha<br/>A. taswira jozi          B. semi<br/>C. istiara                 D. chuku</p> | <p>36. Huenda wahusika wote wawili ni<br/>A. wakulima              B. wanagenzi<br/>C. wafanyabiashara    D. watalii</p> <p>37. Chagua neno lingine lenye maana sawa na 'sahibu'<br/>A. hasidi                  B. mwendani<br/>C. adui                    D. mkufunzi</p> <p>38. Mwandishi wa barua hii anaishi katika eneo la<br/>A. Mpoto                  B. Mizeituni<br/>C. Rahatule               D. Borauhai</p> <p>39. Pia mwandishi angetamatisha pale chini kwa maneno haya ila, wako wa<br/>A. chanda na pete        B. ulimi wa mate<br/>C. mbingu na ardhi      D. uta na upote</p> <p>40. Mwandishi alikusudia kuikamilisha methali hii vipi; Achanikaye kwenye mpini.....<br/>A. hula mbivu             B. hali wali mkavu<br/>C. huls na wakwao      D. hafi njaa</p> |
|--|--|

**Soma ufahamu ifuatayo kisha ujibu maswali 41 – 50.**

Ilikuwa muda wa saa tisa mchana wakati taifa la Kenya lilipofunika na wingu jeusi pi kama kaniki. Nakumbuka siku yenyewe kama jana. Tukio hili la kigaidi lililotekelezwa na magaidi wa kundi la Alshabaab kamwe halitafutika akilini mwangu daima dawama.

Shughuli ziliendelea kama ilivyo desturi, wafanya biashara, wateja wote waliuza na kununua bila fadhaa yoyote ile. Watu walimiminika katika hoteli ya Dusit D2 kama inavyofahamika. Ghafla bin vuu tandabelua, mshikemshike, kivangaito kikazuka bila tahadhari yoyote. Mlipuaji wa kujitolea mhanga akaanzisha hali hii ya kulaaniwa kote ulimwenguni. Kweli mambo ni kangaja huenda yakaja.

Magaidi wakaingia na kuanza kufyatulia binadamu yeyote yule risasi. Wengine ikawa mguu niponye huku wengine wakitambaa ardhini. Wapo waliopiga ukemi, wengine kushtuka na kuzimia nao wengine wakavifunga vyumba walimokuwemo ndi na kunyamaza ji bila kutoa sauti yeyote ile.

Baada ya mashambulizi kutulia idadi ya watu kumi na watano walikuwa wamekata kamba. Majeruhi walikimbizwa katika hospitali za "MP Shah, Avenue na hospitali ya Agha Khan. Hali iliwaendelea mvange baadhi ya majeruhi hivyo basi wakakata kamba.

Idadi kulingana na takwimu inaonyesha kuwa zaidi ya watu ishirini walipoteza maisha yao. Ingawa magaidi hawa walisemekana kuuawa wote, walitusababishia hasara isiyo na kifani.

Heko wananchi wazalendo wa Kenya kwa msaada mliotoa wa damu, vyakula, mablanketi na mamilioni ya pesa kuwasaidia walioathirika. Tuzidishe utu huo kwa kuwa udugu ni kufaana si kufanana.

Wananchi tukufu wa Kenya, tusijali kabila, rangi dini wala tabaka, tuzidi kujitolea kwa hali na mali na Mungu atawajalia neema sufufu kwani hamsahau mja wake asilani.

- |   |  |
|---|--|
| <p>41. Wakati unaozungumziwa ni upi katika aya ya kwanza</p> <p>A. alasiri                      B. dhuha</p> <p>C. Magharibi                  D. aduhuri</p> <p>42. Mwandishi anasema "wingu jeusi pi" hii ni tamathali gani la lugha</p> <p>A. tashbihi                      B. tashhisi</p> <p>C. tanakali ya sauti          D. tashididi</p> <p>43. Shughuli zilibadilika ghafla wakati ambapo</p> <p>A. ufyatulianaji wa risasi ulianza</p> <p>B. mlipuaji wa kujitolea alijilipua</p> <p>C. watu walikosa maakuli yao mkahawani</p> <p>D. damu ilitapakaa kote</p> <p>44. Magaidi ni</p> <p>A wazalendo                      B. waovu</p> <p>C. majangili                      D. wenye utu</p> <p>45. Aya ya tatu inaweza kukamilisha kwa semi gani</p> <p>A. onea gere</p> <p>B. enda shwari</p> <p>C. shika roho mkononi</p> <p>D. kula kalenda</p> | <p>46. Huenda silaha hizi zote zilishuhudiwa katika tukio la mkasa huu ila</p> <p>A. bombomu                      B. kifaru</p> <p>C. manowari                      D. singe</p> <p>47. Wakenya walisaidia wahasiria kwa kuwatolea damu angaa kuwanusuru. Wakati mtu anapotoa damu hupewa malipo yaitwayo</p> <p>A. fidia                              B. arshi</p> <p>C. arbuni                              D. fungule</p> <p>48. Ukarimu wa Wakenya ulidhihirika wakati</p> <p>A. walishuhudia janga lile</p> <p>B. walipowaombea kwa mwenyezi Mungu</p> <p>C. toa mchango wa kifedha mlo na vifaa</p> <p>D. saka na kuwaua magaidi</p> <p>49. Udugu ni kufaana si kufanana' methali hii inatuhimiza</p> <p>A. tuwe watu wanaosaidia wenzetu</p> <p>B tuwe na ubaguziz tunapota michango yetu</p> <p>C. tuwape msaada wale wanaotupa pekee</p> <p>D. tusijishughulisha na lolote lile panapotokea janga</p> <p>50. Taarifa hii inatuonya kutokuwa na</p> <p>A. uzalendo                              B. ukatili</p> <p>C. udugu                                      D. ushirika.</p> |
|---|--|